# HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA

*(Barua zote ziandikwe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji)*

**MKOA WA KILIMANJARO**

*Simu Na.2757652*
*Fax No. 2756463*

**Mkurugenzi Mtendaji**
**S.L.P 176**
**MWANGA**

**25.07.2018**

**TANGAZO LA MARUDIO AWAMU YA PILI KWA AJILI YA KUPATA WAZABUNI TARIJALI KWA AJILI YA KUTOA HUDUMA MBALIMBALI /UKUSANYAJI WA MAPATO NDANI YA HALMASHAURI YA MWANGA KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

(1) Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga anawatangazia Wafanyabiashara. Wananchi, Wakandarasi wote wenye sifa na uwezo wa kutoa huduma mbalimbali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19 watume maombi yao kulingana na mahitaji yaliyoainishwa hapa chini:-

| S/NO | NAMBA YA HUDUMA | MAELEZO YA HUDUMA INAYOHITAJIKA |
|---|---|---|
| 1. | LGA.048/**2018/2019**/G/3 | UTOAJI WA HUDUMA YA MATENGENEZO YA MILANGO NA MADIRISHA YA ALUMINIAMU,NA SAMANI ZA OFISI. |
| 2. | LGA.048/**2018/2019**/G/5 | HUDUMA YA VIFAA VYA KILIMO NA PEMBEJEO |
| 3. | LGA.048/**2018/2019**/C/6 | HUDUMA YA UPIMAJI VIWANJA |
| 4. | LGA.048/**2018/2019**/NCS/7 | HUDUMA YA UDALALI |
| | | |

**ZABUNI ZA WAKALA WA UKUSANYAJI WA USHURU**

| | | |
|---|---|---|
| 5. | LGA.048/**2018/2019**/NCS/11 | UKUSANYAJI WA USHURU SOKO LA BIDHAA MWANGA NA SOKO LA BIDHAA KISANGARA |
| 6. | LGA.048/**2018/2019**/NCS/12 | UKUSANYAJI WA USHURU WA MAEGESHO NA PIKIPIKI |
| 7 | LGA.048/**2018/2019**/NCS/19 | UKUSANYAJI WA USHURU WA MAZAO YA BIASHARA YANAYOTOKA NDANI YA WILAYA |
| 8. | LGA.048/**2018/2019**/NCS/20 | UKUSANYAJI WA USHURU WA SAMAKI UKANDA WA BWAWA WA NYUMBA YA MUNGU- (KIJIJI CHA HANDENI ,LANGATA BORA,KAGONGO,NYABINDA, KITI CHA MUNGU NA NJIA PANDA) |
| 9. | LGA.048/**2018/2019**/NCS/21 | UKUSANYAJI USHURU WA UVUNJWAJI WA SHERIA NDOGO |

(2) Dhana ya pre-qualification Notice kama ilivyoainishwa kwenye sheria ya manunuzi ni kupata watoa huduma Wakandarasi na Wafanya Biashara (Suppliers) wenye uwezo watakaoo kamilisha masharti yaliyoainishwa kuweza kutoa huduma ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

(3) Tangazo hili la kupata Wazabuni tarajali liko wazi kwa Suppliers/Contractors and Service Providers kuomba kulingana na aina biashara anayoiona anaiweza.

(4) Pre-qualification itafanyika kwa ajili ya ushindani wa ki-taifa (National Competitive bidding procedure specified in the Public Procurement (Goods, works, Non-Consultant Services and Disposal of Public Assets by tender) Regulation 2013 pamoja na mabadiliko yake ya mwaka 2016.

(5) Wakandarasi Wafanyabiashara wote watakaopenda kuomba ni lazima waambatanishe pamoja na hati za kisheria zote za uhalali wa biashara husika na ni vyema kuambatanisha Company Profile ya Kampuni husika – VAT, TIN, Leseni, CRB, daraja 7 kuendelea.

Viambatanisho:

- Memorandum and articles of Association
- Authorized Power of Attorney
- Certificate of Incorporation
- Curriculum Vitae of the Management staff
- Kwa makampuni taarifa ya fedha (Bank statement ya kuanzia Julai 2017 hadi machi 2018.
- Tax clearance Certificate.
- Bid security declaration iliyojazwa na kusainiwa kikamilifu.
- Form of Integrity iliyojazwa na kusainiwa kikamilifu.

(6) Mwombaji atatakiwa kuorodhesha kazi alizokwisha fanya na anazoendelea kufanya kwa kipindi cha miaka 3 iliyopita na thamani ya kazi na vyeti vya kukamilisha kazi {Completion Certficate} kwa zile zilizokwisha kamilika.

(7) Wazabuni ni lazima ainishe bayana ilipo Ofisi yake Plot no. Jina la Mtaa.

(8) Kwa watakaoomba ukusanyaji ushuru ni lazima ataje kiwango atakacholipa Halmashauri na Asilimia ya marejesho yake kama Fomu ya maoteo inavyoelekeza kama akishinda zabuni husika.

(9) Usafi katika masoko ni jukumu la Mzabuni atakayeshinda zabuni hiyo /Halmashauri haitahusika kikivyote kuwalipa watumishi au vibarua wa wakala wa ukusanyaji ushuru.

(10) Mwombaji wa zabuni kwa ajili ya wakusanyaji ushuru lazima kuwa na Perfomance Bond isiyo pungua mara mbili ya thamani ya zabuni atakayoomba au Security Bond isiyo pungua mara mbili ya thamani ya zabuni.

(12) Tathimini itazingatia Masharti yaliyoainishwa kwenye Tangazo na Kitabu cha Zabuni husika.

(13) Mwisho wa kutuma maombi ni Ijumaa tarehe 10.08.2018 saa 4.30 kamili asubuhi. Maombi yote yakiwa yamefungwa kwenye bahasha yenye lakiri na isiyo na alama ya kumtambulisha aliyeomba. Yanatakiwa yawe yameshatumwa kwa Register au kuletwa kwa mkono kwenye Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Mwanga iliyopo Ofisi ya Makao Makuu ya Halmashauri S.L.P. 176 Mwanga, kabla na si zaidi ya saa 4.30 Asubuhi tarehe 10.08.2018 na ufunguzi utafanyika mara tu mwisho wa saa na tarehe tajwa hapo juu kukamilika.

(14) Kila atakayeomba ni lazima aonyeshe namba na maelezo ya Huduma aliyoomba juu ya bahasha na aonyeshe kwa maandishi isifunguliwe hadi tarehe 10.08.2018 ieleweke kuwa asipoainisha aina ya Huduma aliyoombea Zabuni hiyo haitafunguliwa.

(15) Zabuni zitakazoletwa baada ya muda kuisha hazitapokelewa na wala kufunguliwa.

(16) Watumishi wa Halmashauri pamoja na Waheshimia Madiwani hawaruhusiwi kuomba Zabuni hizi.

(17) Ada ya mchakato huu wa Wazabuni tarijali ni shilingi za Kitanzania Elfu hamsini tu 50,000/= ambazo hazirejeshwi. Na zinapaswa kulipwa kwenye Ofisi ya Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu jioni siku za kazi, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kwa kila zabuni utakayoomba inajitegemea.

**GOLDEN A. MGONZO**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**MWANGA**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MWANGA